**NOVENA KWA MTAKATIFU MONIKA.**
**Shirika la Mtakatifu Agustino Tanzania.**




## YALIYOMO:


| | | |
|---|---|---|
| Utangulizi | …………………………………. | 02 |
| Umuhimu wa Novena hii | …………………………………. | 02 |
| Je, Umekata Tamaa ? | …………………………………. | 02 |
| Siku ya Kwanza (1) | …………………………………. | 03 |
| Siku ya Pili (2) | …………………………………. | 04 |
| Siku ya Tatu (3) | …………………………………. | 05 |
| Siku ya Nne (4) | …………………………………. | 06 |
| Siku ya Tano (5) | …………………………………. | 07 |
| Siku ya Sita (6) | …………………………………. | 08 |
| Siku ya Saba (7) | …………………………………. | 09 |
| Siku ya Nane (8) | …………………………………. | 10 |
| Siku ya Tisa (9) | …………………………………. | 11 |
| Litania kwa Mtakatifu Monika | …………………………………. | 12 |

**Utangulizi**
Mtakatifu Monika alizaliwa katika Familia ya Kikristo huko Tagaste, Nchi iitwayo sasa Algeria, katika Afrika ya Kaskazini, Mwaka 332 (Baada ya Kristo). Aliolewa na Mwanaume Mpagani aliyeitwa Patrisio, akabarikiwa kupata Watoto watatu, miongoni mwao alikuwamo Agustino.

Kwa vile Patrisio hakuwa Mwanaume wa mfano na mwenye Fadhila, Monika alisali sana akimwombea Uadilifu na Uongofu wa Kweli. Kutokana na Utakatifu, Udumivu katika Sala na Uvumilivu wa Monika, Patrisio alibatizwa Mwaka mmoja kabla ya Kifo chake.

Upande mwingine Monika alidumu katika kumwombea Mtoto wake Agustino, Mtoto aliyefuata Maelekeo Mabaya ya Baba yake. Kwa Miaka mingi Monika alilia kwa Njia ya Sala kwa ajili ya Uongofu wa Mwanaye Agustino. Mungu alimsikiliza na mwisho akapokea Sala zake. Mwisho Agustino aliongoka, alibatizwa na Mtakatifu Ambrosi, Askofu wa Milani, katika Vigilia ya Pasaka Mwaka 387 (Baada ya Kristo). Monika alifariki kwa Amani akiwa na Umri wa Miaka 56, huku akifurahia Uongofu wa Mwanaye. **Apumzike kwa Amani.**

**Umuhimu wa Novena hii**
Kutokana na Umuhimu wa Mtakatifu Monika, Shirika la Mt. Agustino linatualika Watu wote Kusali kwa ajili ya Mahitaji mbalimbali ya Mwili na Roho kama ifuatavyo:

- Kwa ajili ya Wazazi wanaosumbuka katika Familia na katika Maisha yao.
- Akina Mama wanaopigwa, Kunyanyaswa na Kuonewa na Waume zao.
- Akina Mama Waliokata Tamaa katika Maisha na katika Ndoa zao.
- Kwa ajili ya Matatizo Magumu ya Kifamilia.
- Wazazi Waliokata Tamaa na Watoto wao.
- Akina Mama Wajane Wanaosumbuka au Kuhangaika na Mirathi, Mfumo wa Kijamii.
- Watu Walioathirika na Pombe na Madawa ya Kulevya.
- Kwa ajili ya Vilema Sugu vya Kiroho na mambo mengine Kadiri ya Mahitaji yako.

**Je, Umekata Tamaa ?**
Hebu mwangalie Mtakatifu Monika, Nyota ya Matumaini, na Mama mwenye Udumivu katika Kusali. Sali kwa Maombezi yake, kwa Imani, kwani Mungu atakusaidia.

*Tumsifu Yesu Kristo ……….*

**Siku ya Kwanza (1)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mungu Baba Mwenyezi wa Milele, nakuja kwako Kusali Novana hii kwa Muda wa Siku Tisa, kwa Maombezi ya Mama yetu Mtakatifu Monika. Najiweka Mikononi mwako, kwa Ibada Kuu, Imani Thabiti na Matumaini yote.

Kumbuka, Ee Mama Mpendwa, Mtakatifu Monika, Furaha iliyojaza Moyo wako wakati Mwanao Agustino, uliyemzaa mara ya pili kwa Njia ya Sala na Machozi mengi, alipogeuza Maisha yake na Kumwongokea Mungu. Nakuomba, Ee Mama Mpendwa sana, nipelekee Maombi ya Novena hii mbele ya Uso wa Mungu wangu, ambaye mbele yake unasimama ukiniombea kama ulivyomwombea Mwanao Agustino, ukafanikiwa.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika ………………… Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino ………………… Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu ………………… Mtuombee**

**Siku ya Pili (2)**

**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Ee Monika, Mwombezi Mkuu wa akina Baba na akina Mama; tafadhali chukua Watoto wetu, uwaweke chini ya Ulinzi wako, hasa Watoto wale waliomwasi Mung una Kanisa lake. Uwaombee ili Daima wawe Waaminifu kwa Viapo vyao vya Ubatizo. Uwape Nguvu ya kutembea Daima katika Njia ya Bwana, ili wavishinde Vishawishi na waepukane na Mitindo Mibaya ya Ulimwengu huu. Uwaombee Daima, ili washiriki nawe Furaha za Uzima wa Milele.

Na sasa, Ee Mama Mtakatifu sana, naomba uniombee kwa Mungu ili nijaliwe yote niombayo. Naamini kuwa Sala zako mbele ya Yesu zina Nguvu ya Pekee. Naomba uniombee kwa Machozi mengi, kama ulivyomwombea Mwanao Agustino, bila Kukata Tamaa hadi akaongoka.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika …………………  Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino …………………  Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu …………………  Mtuombee**

**Siku ya Tatu (3)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mtakatifu Monika, baada ya Muda Mrefu wa Sala ya Machozi mengi, Kufunga na kutoa Sadaka; ulipata Furaha ya kushuhudia Uongofu wa wote wawili:- Mumeo na Mwanao.

Baada ya Mwanao Agustino kurudi kwenye Imani ya Kanisa Katoliki ulisema: “Mungu amenijalia haya yote zaidi ya niliyoomba. Nisubiri kufanya nini tena ?” Siku chache baadaye uliaga Dunia kwa Furaha na Amani katika Mungu.

Uniombee, Ee Mtakatifu Monika, ili niwe na Amani na Imani, ili niweze kupokea Mapenzi ya Mungu kama wewe ulivyofanya. Mwisho wa haya yote, unijalie niishi Muda wote bila Dosari, na hatimaye nifike Salama kwenye Nyumba yetu ya Mbinguni.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika ………………… Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino ………………… Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu ………………… Mtuombee**

**Siku ya Nne (4)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mtakatifu Monika, unaona katika Ulimwengu wetu wa leo, akina Mama wengi na Wanawake katika Ndoa Wanavyohangaika na Kuteseka kwa sababu ya Wanaume na Watoto wao. Unajua vizuri namna gani wanajisikia, kwa sababu wewe mwenyewe ulipitia Mateso kama hayo; lakini uliyashinda yote. Zaidi ya hayo, uliamini kuwa, Matatizo ya Mume wako na Mwanao, ni Changamoto uliyopewa na Mungu.

Uliteseka sana, na hata hivyo, uliwaombea Mumeo na Mwanao bila kukoma. Mungu aligusa Moyo wa Mumeo Patrisio na Mwanao Agustino. Utuombee nasi Ujasiri kama huo na Imani kama yako, ili tuweze Kusali kwa Mungu bila Kukoma hadi atakapopokea Sala zetu.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika …………………  Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino …………………  Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu …………………  Mtuombee**

**Siku ya Tano (5)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mtakatifu Monika, tunaweka mbele yako Maisha ya akina Mama wanaofanya Kazi Nje ya Nchi, wakitafuta Maisha Bora kwa ajili ya Familia zao. Wanalala kila Siku wakikukumbuka wewe uliye Mwombezi wa akina Mama wanaopigwa na Waume zao na Wanawake Waliokata Tamaa katika Ndoa. Akina Mama hawa wanawakumbuka pia Waume na Watoto wao, wakitamani kuwa karibu nao.

Lakini ni Lazima watolee Sadaka Kubwa, ili Watoto wao waende Shule na wawe na Maisha Mazuri ya baadaye. Tunakuomba Uwalinde akina Mama hawa, na uwajalie Watoto wao, Hekima na Akili ili wasome kwa Bidii.

Tunaomba Maombi yako ili Wanaume na Watoto wa akina Mama hawa, waweze kuwasiliana kwa Njia mbalimbali na hivyo, kuondoa Ukuta wa Umbali uliopo kati yao. Tunawaombea sana ili Maumivu ya Umbali na Mipaka kati yao, visiwe Kikwazo kwa Familia zao Kuishi kwa Amani na Furaha.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika ………………… Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino ………………… Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu ………………… Mtuombee**

**Siku ya Sita (6)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mtakatifu Monika, ulifanya Kazi Kubwa kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Agustino; ili waweze kuingia katika Ufalme wa Mbinguni. Mbingu ilikuwa Matamanio na kila kitu kwako. Ulisafiri mbali kumtafuta Mwanao Agustino, Ukasali Masaa mengi, kwa sababu Ulitamani sana Familia yako ifike Mbinguni.

Mafanikio ya Dunia hii hayakukuvutia kabisa. Hata Akili nyingi na Uwezo Mkubwa wa Mwanao Agustino, havikukufanya upoteze Matamanio ya Mbinguni. Ulitaka Mwanao atumie Muda wake wote na Karama zake zote, ili kuandaa Makao ya Mbinguni; na hicho ndicho wewe na Mwanao Agustino mlikifanya.

Usikilize Hima Sala yangu ya Novena hii, ili Wazo la kwenda Mbinguni liwe Matamanio yangu zaidi ya vitu vyote. Uniombee, ili nisiruhusu Mafanikio ya Dunia hii yapofushe Macho yang una hivyo, kushindwa Kuona Njia ya kufika Mbinguni, bali uniongoze kwa Yesu na uniandae kukutana na Yesu Mbinguni. Amina.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika ………………… Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino ………………… Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu ………………… Mtuombee**

**Siku ya Saba (7)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mtakatifu Monika, Mwanao Agustino alipokumbuka Hatua zake kuelekea Kuongoka, hakusahau Machozi na Sala zako. Agustino alikuona ukikaa Macho Usiku kucha, Ukisali ili Mungu aguse Moyo wake, na hivyo aweze Kutubu Dhambi zake. Agustino alielezea Kuongoka kwake kuwa ilikuwa Kazi Kubwa yakow ewe Mama yake, kiasi kwamba hata Mungu hakuweza kufumbia Macho Uadilifu na Udumivu wako katika Sala.

Ukiwa Mbinguni tunajua kuwa Yesu anakusikiliza, na hataweza kutupilia mbali Sala zako. Nakusihi sana, unifanye Mwanao Agustino wa leo kwa Kuniombea ili nami niweze Kuongoka kutoka Mienendo isiyofaa na Daima niishi Maisha ya Utakatifu.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika ………………… Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino ………………… Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu ………………… Mtuombee**

**Siku ya Nane (8)**

**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**

Ee Mtakatifu Monika, ulimsindikiza Mwanao Agustino alipoanza Safari ya Maisha ya Uongofu hadi Ubatizo wake. Ulizama katika Maisha ya Sala na ulifurahi kwamba Mwanao alifanya Uamuzi wa Busara kuchagua Njia hiyo ya Utakatifu.

Hata wewe Mama Monika, ulipenda kutumia Muda wa Maisha yako yote, Ukisali na ukiwa karibu kabisa na Yesu. Utusaidie ili nasi tuweze kuzama katika Maisha ya Sala na kufanya Sala sehemu ya Maisha yetu.

Njia ya kuelekea Maisha ya Sala inaanza pale ambapo Mioyo yetu hutulia, na Tamaa za mambo ya Dunia hii zikiwa zimekufa kabisa ndani yake. Hapo ndipo tunaingia katika Maisha ya Sala, Imani, Unyenyekevu, na Kuungama kabisa na Mungu; Maisha ambayo wewe na Mwanao mliyaishi.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika ………………… Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino ………………… Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu ………………… Mtuombee**

**Siku ya Tisa (9)**
**Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.**
Ee Mtakatifu Monika, katika Siku ya Mwisho ya Novena hii, naleta kwako Mahitaji ya akina Mama wanaohangaika, akina Mama ambao hawajajiandaa kuwa Wazazi ili uwaombee na kuwa Msaidizi katika Maisha yao. Tunasali pia kwa Maombezi yako, uliye Kielelezo cha Sala, Utuombee ili tuepukane na Mimba zisizo Kubwa katika Jamii yetu. Vijana na Watu wengi wanamwasi Mungu kwa sababu ya Tatizo hili.

Uwaangazie Vijana wetu, na uwape Walimu Wazuri wa kuwafundisha Kuheshimu Miili yao na hivyo kutofanya Tendo la Ndoa kabla au Nje ya Ndoa. Wasali Novena hii kwa Maombezi yako ili wajilinde na Udanganyifu na Hila za yule Mwovu. Uwape Ufahamu na Hekima ya Kufurahia Ujana wao bila kutenda Dhambi, na uwaongoze kwenye Furaha ya Kweli isiyo na Mwisho; huko unakoishi na Mungu wetu, Daima na Milele. Amina.

- Ee Mpendwa sana, Mama Mtakatifu Monika, Mama uliyesumbuka sana, na ambaye Mateso mengi yaliuumiza Moyo wako wakati wa Uhai wako hapa Duniani; Njoo Hima Unisaidie Mwanao katika Mahangaiko yangu.

- Pamona na Maumivu na Mateso yote uliyopata, Hukukata Tamaa, wala hukupoteza Imani yako kwa Mungu; bali kwa Ujasiri Mkubwa, ukidumu katika Sala, na Imani Thabiti; Ulisali kila Siku kwa Machozi mengi, kwa ajili ya Uongofu wa Mumeo Patrisio na Mwanao Mpendwa Agustino. Kwa Ujasiri huo Mungu alisikia Sala yako, na hivyo Mumeo na Mwanao waliongoka.

- Uniombee Ujasiri kama huo, Uvumilivu, Udumivu katika Sala na Imani Thabiti kwa Bwana. Uniombee, Ee Mpendwa Mama Mtakatifu Monika, ili Mungu asikie Kilio change ***(hapa taja Ombi lako unalomwomba Mungu kwa Maombezi ya Mtakatifu Monika).***

- **Baba yetu (3), Salamu Maria (3), Atukuzwe Baba (3)**
- **Mtakatifu Monika …………………  Utuombee**
- **Mtakatifu Agustino …………………  Utuombee**
- **Watakatifu wote wa Mungu …………………  Mtuombee**

**Litania kwa Mtakatifu Monika**

Bwana Utuhurumie …………… Bwana Utuhurumie
Kristo Utuhurumie …………… Kristo Utuhurumie
Bwana Utuhurumie …………… Bwana Utuhurumie

……………………………………………………………………………………………

Baba wa Mbinguni, Mungu …………… Utuhurumie
Mwana Mkombozi wa Dunia, Mungu …………… Utuhurumie
Roho Mtakatifu, Mungu …………… Utuhurumie
Utatu Mtakatifu, Mungu mmoja …………… Utuhurumie

……………………………………………………………………………………………

Maria, Mama wa Yesu na Mama yetu …………… Utuombee
Maria, Mama yetu wa Faraja …………… Utuombee
Maria, Mama yetu wa Shauri Jema …………… Utuombee
Maria, Nguvu katika Udhaifu wetu …………… Utuombee
Maria, Mwanga katika Giza letu …………… Utuombee
Maria, Ushindi katika Vishawishi vyetu …………… Utuombee
Maria, Unayetuunganisha na Yesu …………… Utuombee
Maria, Mwombezi Mpenzi wa Mt. Agustino …………… Utuombee

……………………………………………………………………………………………

Mt. Monika, Mama Mwombezi wa Mwanaye Agustino …………… Utuombee
Mt. Monika, Mama Mtaratibu …………… Utuombee
Mt. Monika, Mama mwenye Uvumilivu …………… Utuombee
Mt. Monika, Mama mwenye Huruma …………… Utuombee
Mt. Monika, Mama mwenye Upendo wa Kweli …………… Utuombee
Mt. Monika, Mama Mdumivu Sala …………… Utuombee

Mt. Monika, Kielelezo cha Uchaji wetu wa Mungu …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo kwa akina Mama Wakristo …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo cha Ujasiri wetu katika Sala …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo cha Kusali bila Kukoma …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo cha Upendo wetu kwa Wakosefu …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo Bora cha Mama wa Familia …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo cha Uvumilivu katika Majaribu …………… Utuombee
Mt. Monika, Kielelezo Bora cha Wajane …………… Utuombee
Mt. Monika, uliyemkabidhi Mungu, Mwanao Agustino …………… Utuombee

Mt. Monika, Kioo cha Uadilifu wetu …………… Utuombee
Mt. Monika, Kioo cha Utakatifu wetu …………… Utuombee
Mt. Monika, Kioo cha Mama Bora wa Familia …………… Utuombee
Mt. Monika, Kioo cha Mke Mwema katika Ndoa …………… Utuombee
Mt. Monika, Malaika Mlinzi wa Mwanaye Agustino …………… Utuombee

Mt. Monika, Malaika Mwombezi wa Mumewe Patrisio …………… Utuombee

Mt. Monika, Shujaa wa Malezi ya Familia …………… Utuombee
Mt. Monika, Shujaa wa Kuwaongoa Wakosefu …………… Utuombee
Mt. Monika, Shujaa katika Kujitoa Sadaka …………… Utuombee
Mt. Monika, Mwombezi wetu mwenye Nguvu …………… Utuombee
Mt. Monika, Mwombezi wa akina Mama Wakristo …………… Utuombee
Mt. Monika, Mpendevu wa Maria Mama wa Faraja …………… Utuombee
Mt. Monika, uliyekufa kwa Furaha …………… Utuombee
…………………………………………………………………………………………………

Mwana Kondoo wa Mungu, Uondoaye Dhambi za Ulimwengu…………...Utusamehe Ee Bwana
Mwana Kondoo wa Mungu, Uondoaye Dhambi za Ulimwengu……………Utusikilize Ee Bwana
Mwana Kondoo wa Mungu, Uondoaye Dhambi za Ulimwengu……………Utuhurumie
…………………………………………………………………………………………………

**Kiongozi:** Umemteua, Ee Bwana, Mtumishi wako Mtakatifu Monika
**Wote:** Ili Daima Atuombee kwako kwa Machozi yasiyokoma.

**Tuombe:** Ee Mungu ambaye ulimteua Mtumishi wako Mtakatifu Monika, ili awe Mwombezi wa Mumewe Patrisio na Mwanaye Agustino kwa Machozi mengi yaliyolowesha kila alipopita hadi wakaongoka wote wawili; Utujalie nasi kwa Maombezi yake, kuacha Yasiyokupendeza na Kuambatana na yale Yakupendezayo wewe Daima. Tunaomba hayo kwa Njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.



**Shirika la Mtakatifu Agustino Tanzania.**

**Allan A.F.M Mseppa**
**allanmseppa@gmail.com**